

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



20 APRILI, 2022



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA TISA – TAREHE 20 APRILI, 2022

**I. DUA**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.



**III. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**73. MHESHIMIWA DEUS CLEMENT SANGU (KWELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itajenga walau KM 3 za barabara ya lami katika Mji wa Laela Sumbawanga ambao hauna barabara ya lami.

**74. MHESHIMIWA MUSSA RAMADHANI SIMA (SINGIDA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itajenga Hospitali ya Wilaya Singida Mjini.

**75. MHESHIMIWA JOSEPHINE GENZABUKE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itamaliza tatizo la ukosefu wa Watumishi wa Kada mbalimbali katika Hospitali nchini pamoja na ukosefu wa Vifaa Tiba.

**OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

**76. MHESHIMIWA DKT. DAVID MATHAYO DAVID (SAME MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-


Je, ni lini Serikali itatoa vibali kuajiri Walimu kukabiliana na ongezeko la Wanafunzi na ni Wahitimu wangapi wapo katika soko la ajira.

#### **WIZARA YA MADINI:**

#### **77. MHESHIMIWA MARGARET SIMWANZA SITTA (URAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, Serikali ina taarifa juu ya Madini yanayopatikana Wilayani Urambo na lini itawasaidia Wananchi wanufaikie na Madini hayo.



#### **WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

#### **78. MHESHIMIWA JONAS VAN ZEELAND (MVOMERO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni lini Serikali itatatura mgogoro wa mpaka kati ya Hifadhi ya Wamembiki na Wananchi wa Vijiji vinavyopakana na Hifadhi hiyo.

## **WIZARA YA NISHATI:**

### **79. MHESHIMIWA JACKSON GEDION KISWAGA (KALENGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Serikali itapeleka transforma yenyewe uwezo mkubwa wa njia tatu katika Kijiji cha Nyamihu Kata ya Nzihi Jimbo la Kalenga.

## **WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

### **80. MHESHIMIWA HAWA SUBIRA MWAIFUNGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

Je, ni lini Serikali italipa fidia Wananchi wa Kijiji cha Usulo Kata ya Mbungani Tabora Manispaa ambao maeneo yao yalichukuliwa na Jeshi.

## **WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

### **81. MHESHIMIWA SELEMANI JUMANNE ZEDI (BUKENE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, nini kinachelewesha ujenzi wa Barabara kutoka Tabora – Mambali – Bukene hadi Kagongwa ilihali ilishatengewa bajeti.

#### IV. HOJA ZA SERIKALI:

##### **WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.



*(Majadiliano yanaendelea)*

DODOMA  
20 APRILI, 2022

N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE

